

OFISI YA TAIFA YA TAKWIMU
SHINDANO LA MWANDISHI BORA WA HABARI ZA TAKWIMU KWA
MWAKA 2022

Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaendelea na maandalizi ya Siku ya Takwimu Afrika ambayo huadhimishwa kila tarehe 18 Mwezi Novemba ya kila mwaka. Kwa mwaka huu, kilele cha Maadhimisho haya yanatarajiwa kufanyika Mkoani Arusha. Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa kutambua umuhimu wa Vyombo vya Habari katika kuelimisha jamii kuhusu shughuli mbalimbali za Kitakwimu, imekuwa ikiandaa Shindano la Waandishi Bora wa Habari za Kitakwimu kila mwaka. Shindano hili lina lengo la kuhimiza unaadishi zaidi wa shughuli za kitakwimu pamoja na kuhimiza matumizi ya takwimu katika majukumu ya kila siku. Hivyo basi, NBS inawaalika Waandishi wa Habari kukusanya kazi zao walizo zifanya kuanzia Januari, 2022 hadi Novemba 10, 2022 ili ziweze kushiriki kushindanishwa na kupata Waandishi Bora watatu kwa mwaka huu.

Shindano hili ni kwa Waandishi walioajiriwa au wakujitegemea wanaofanya kazi na *Taasisi mbalimbali ikiwemo vyombo vya Habari vya Magazeti, televisheni, redio na mitandao ya kijamii ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

Makala/Habari zitakazopokelewa kwa ajili ya shindano hili ni zile zilizochapishwa magazetini na kwenye mitandao inayochapisha habari katika kipindi kilichotajwa kati ya Januari hadi Novemba, 2022.

VIGEZO NA SIFA ZA MAKALA/HABARI ZITAKAZO SHINDANISHWA

1. Makala/Habari husika iwe ya uchambuzi wa kina wa mada inayochambua kilichomo kwenye takwimu na iwe kwenye lugha rahisi inayoeleweka kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza;
2. Lugha ya picha inatakiwa iwe rahisi wakati wa kuelezea maudhui ya kilichowasilishwa;
3. Inapaswa kujumuisha vyanzo vya kuaminika vya habari ili kuongeza

thamani/ladha ya habari inayoelezea takwimu hizo;

4. Makala/Habari iwe yenye Ushahidi wa Takwimu ambazo zimeandaliwa na mwandishi kwa kuchambua na kuhoji ripoti rasmi ya takwimu (Statistical Report) ili kupata taarifa au ujumbe zaidi uliokusudiwa katika jamii.
5. Makala/ Habari inapaswa itoe takwimu zenye malengo ya kibinadamu/kumgusa mtu au jamii. Inapaswa izingatie ubinadamu na kujibu swali, kwa nani tunajali?
6. Inabidi iwe na mchanganyiko wa maandishi, habari picha na vielelezo vyote ambavyo vitamfanya mtu aelewe dhumuni la ujumbe na achukue hatua kutokana na Ushahidi wa takwimu zilizotolewa.

Washiriki wawasilishe kazi zao kabla ya tarehe 16 Novemba 2022, saa kumi jioni. Kupitia barua pepe ifuatayo: takwimutanzania@gmail.com

Kwa maelezo zaidi wasiliana na **William Matee** kwa namba **0716 621 067** au **Emmanuel Ghula** kwa namba **0756 934 356**.

Tangazo hili limetolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu.